TANGAZO LA SERIKALI NA. 758 la tarehe 27/10/2023

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,
(SURA YA 415)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 28(3))*

AMRI YA TOZO ZA BANDARI ZA BAHARI NA MAZIWA YA MWAKA 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itaitwa Amri ya Tozo za Bandari za Bahari na Maziwa ya Mwaka 2023. na itaanza kutumika siku thelathini baada ya tarehe ya kuchapishwa katika gazeti la serikali.

Matumizi

2. Amri hii itatumika wakati Mamlaka inapotoa huduma katika bandari za bahari na bandari za maziwa.

Tafsiri

3. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo:

Sura ya 166

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Bandari;

Sura ya 415

"Shirika" maana yake ni Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lililoanzishwa chini ya Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;

"mtoa huduma anayedhibitiwa" maana yake ni mtu mwenye leseni ya kutoa huduma inayodhibitiwa; na

TS. Na. 7 la mwaka 2020

"tozo" ina maana kama ilivyotafsiriwa kwenye Kanuni za Tozo. za Wakala wa Meli.

*Tangazo La Serikali Na. 758 (Linaendelea)*

## SEHEMU YA PILI
## TOZO NA MASHARTI YANAYOTUMIKA

Tozo zilizoidhinishwa

4. Wakati wa kutoa huduma za bandari, Mamlaka itahakikisha kuwa -
(a) bahari, inatoza tozo isiyozidi kiwango kilichoidhinishwa katika Jedwali la Kwanza la Amri hii; au
(b) iwapo ni bandari za maziwa, inatoza tozo isiyozidi kiwango kilichoidhinishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii.

Masharti ya huduma

5. Wakati wa kutoa huduma, Mamlaka itazingatia masharti yafuatayo:
(a) inandaa na kuwasilisha kwa Shirika vitabu vya tozo za bandari za bahari na maziwa kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika aya ya 4 ndani ya kipindi cha siku kumi na nne tangu kuchapishwa kwa Amri hii;
(b) inatoa taarifa za kutosha kwa watumiaji wa bandari kuhusu mawanda ya huduma inayotolewa;
(c) haitoi leseni kwa mtoa huduma anayedhibitiwa;
(d) inatoza tozo ya ufunguaji na ufungaji wa mifuniko ya gamla kwa bandari za maziwa endapo wafanyakazi au mitambo ya Mamlaka imetumika utoahi huduma hiyo;
(e) inatoza tozo ya kuinua shehena nzito inayotembea kwa kutumia matairi yake yenyewe endapo shehena hiyo inahitaji uangalizi wa kipekee wa Mamlaka wa kuwezesha upakiaji au ushushaji wa shehena hiyo melini ikijumuisha ukokotaji;
(f) inafanya tathmini na kuandaa mpango utakaoonesha usimikaji wa vifaa vya kuhudumia shehena pamoja na miundombinu ya kupakia na kushusha wanyama melini katika bandari za maziwa na kuuwasilisha kwa Shirika ndani ya

miezi sita tangu kuchapishwa kwa Amri hii;

(g) inazingatia maelekezo ya Benki Kuu ya Tanzania kuhusu matumizi ya fedha za kigeni Nchini kwa lengo la kuwezesha malipo ya huduma za bandari kufanyika kwa fedha ya kitanzania;

(h) inaimarisha mikakati ya kimasoko ili kuvutia shehena zaidi kupita katika bandari za bahari na maziwa Nchini;

(i) inatoa uelewa kwa watumiaji wa huduma za bandari kuhusu tozo za bandari zilizoidhinishwa;

(j) inaruhusu abiria katika bandari za maziwa kusafiri na mzigo wa samaki usiozidi kilogramu ishirini bila tozo;

(k) kutowatoza wateja watumiao miundombinu ya kupitisha mafuta ya Kigamboni; na

TS Na. 459 la mwaka 2022

(l) inazingatia maagizo ya Amri ya Tozo za Bandari Kavu za Wakala wa Meli za Mwaka 2022.

---

**JEDWALI LA KWANZA**

---

*(Limetengenezwa chini ya aya 4(a))*

**TOZO ZA KIKOMO ZA BANDARI ZA BAHARI**

| Tozo | Kipimo cha Tozo | Kiwango cha Tozo (Bila VAT) |
|---|---|---|
| Kukodi boti ya muingiza meli bandarini | saa moja au sehemu yake | USD 500 |
| Kemikali/mapovu ya kuzimia moto | lita moja | USD 15 |
| Ukaguzi wa forodha | kasha linaloishia Nchini lisilozidi futi 20 | USD 90 |
| | kasha linaloishia Nchini linalozidi futi 20 | USD 140 |
| | kasha linalopita kwenda nchi | USD 80 |

Tangazo La Serikali Na. 758 (Linaendelea)

| Tozo | Kipimo cha Tozo | Kiwango cha Tozo (Bila VAT) |
|---|---|---|
| | jirani lisilozidi futi 20 | |
| | kasha linalopita kwenda nchi jirani linalozidi futi 20 | USD 140 |
| Tozo ya matumizi ya gati la bandari kwa kasha linalopita kwenda nchi jirani | kasha linalopita kwenda nchi jirani lisilozidi futi 20 | USD 90 |
| | kasha linalopita kwenda nchi jirani linalozidi futi 20 | USD 180 |
| | kasha linalopita kutoka nchi jirani lisilozidi futi 20 | USD 75 |
| | kasha linalopita kutoka nchi jirani linalozidi futi 20 | USD 150 |
| Tozo ya matumizi ya gati la bandari kwa shehena isiyotoka bandarini kwa bandari za Tanga na Mtwara | kasha lisilozidi futi 20 | haihusiki |
| | kasha linalozidi futi 20 | haihusiki |
| Tozo ya matumizi ya gati la bandari kwa shehena mchanganyiko isiyotoka bandarini) kwa bandari za Tanga na Mtwara | tani ya kibandari | USD 2 |
| Upimaji wa uzito wa kasha katika bandari za Tanga na Mtwara | kasha | USD 30 |
| Malipo ya ziada kwa shehena hatarishi | asilimia ya tozo ya kupakia au kushusha shehena | asilimia kumi ya tozo ya kupakia au kushusha shehena |
| | asilimia ya tozo ya uhamishaji wa shehena kati ya gati na maeneo ya uhifadhi au chombo cha usafirishaji katika nchi kavu | asilimia kumi ya tozo ya uhamishaji wa shehena kutoka au kwenda katika gati |
| | asilimia ya gharama za uhifadhi | asilimia ishirini ya gharama za uhifadhi |
| **Angalizo:** Tozo nyingine ambazo hazijatajwa katika Jedwali hili zinaidhinishwa kama zilivyo katika Maombi yenye Kumb. Na.: JA.570/671/01-E/31 ya tarehe 22 Mei, 2023 kuhusu Tozo za Bandari za Bahari yaliyowasilishwa kwa Shirika kwa mujibu wa *kanuni ya 8(1) ya Kanuni za Tozo,* TS. Na. 7 la mwaka 2020. | | |

**JEDWALI LA PILI**

*(Limetengenezwa chini ya aya 4(b))*

**TOZO ZA KIKOMO ZA BANDARI ZA MAZIWA**

| **Tozo** | **Kipimo cha Tozo** | **Kiwango cha Tozo (Bila VAT)** |
|---|---|---|
| Tozo ya kupakia au kushusha shehena kwa kreti tupu | tani ya kibandari | USD 1.5 |
| Tozo ya matumizi ya gati la bandari kwa kreti tupu | tani ya kibandari | USD 1 |
| Tozo ya uhamishaji wa moja kwa moja wa shehena kati ya gati na chombo cha usafirishaji katika nchi kavu kwa shehena ya kreti tupu | tani ya kibandari | USD 2 |
| Tozo ya uhamishaji wa shehena kati ya gati na maeneo ya uhifadhi au chombo cha usafirishaji katika nchi kavu kwa shehena ya kreti tupu | tani ya kibandari | USD 3 |
| Tozo ya kufunga meli na matumizi ya vifaa vya kuongoza meli bandarini kwa meli iliyosajiliwa Tanzania | kwa siku kwa meli yenye urefu usiozidi mita 15 | USD 6 |
| | kwa siku kwa meli yenye urefu wa kati ya mita 16 na mita 50 | USD 12 |
| | kwa siku kwa meli yenye urefu wa kati ya mita 51 na mita 70 | USD 16 |
| | kwa siku kwa meli yenye urefu wa kati ya mita 71 na mita 90 | USD 20 |
| | kwa siku kwa meli yenye urefu wa zaidi ya mita 90 | USD 24 |
| Tozo ya kufunga meli iliyosajiliwa Tanzania kwa ajili ya kusubiri shehena bandarini | asilimia ya tozo ya kufunga meli | asilimia kumi na tano ya tozo ya kufunga meli |
| Tozo ya kufunga meli | asilimia ya tozo ya kufunga | asilimia ishirini |

*Tangazo La Serikali Na. 758 (Linaendelea)*

| **Tozo** | **Kipimo cha Tozo** | **Kiwango cha Tozo (Bila VAT)** |
| --- | --- | --- |
| iliyosajiliwa nje ya nchi kwa ajili ya kusubiri shehena bandarini | meli | ya tozo ya kufunga meli |
| Tozo ya kufunga meli na matumizi ya vifaa vya kuongoza meli bandarini<br>kwa meli iliyosajiliwa Tanzania katika bandari ndogo katika maziwa | kwa mwezi kwa meli yenye urefu usiozidi mita 10 iliyowasili mara moja | TZS 8,000 |
| | kwa mwezi kwa meli yenye urefu usiozidi mita 10 iliyowasili angalau mara mbili | TZS 16,000 |
| | kwa mwezi kwa meli yenye urefu wa kati ya mita 11 na mita 15 iliyowasili mara moja | TZS 16,000 |
| | kwa mwezi kwa meli yenye urefu wa kati ya mita 11 na mita 15 iliyowasili angalau mara mbili | TZS 32,000 |
| | kwa mwezi kwa meli yenye urefu wa zaidi ya mita 15 iliyowasili mara moja | TZS 20,000 |
| | kwa mwezi kwa meli yenye urefu wa zaidi ya mita 15 iliyowasili angalau mara mbili | TZS 40,000 |
| | tozo ya kufunga meli kwa dharura | TZS 5,000 |
| **Angalizo:** Tozo nyingine ambazo hazijatajwa katika Jedwali hili zinaidhinishwa kama zilivyo katika Maombi yenye Kumb. Na.: JA.570/671/01-E/31 ya tarehe 22 Mei, 2023 kuhusu Tozo za Bandari za Maziwa yaliyowasilishwa kwa Shirika kwa mujibu wa *kanuni ya 8(1) ya Kanuni za* Tozo, TS. Na. 7 la Mwaka 2020. | | |

Dar es Salaam,
22 Octoba, 2023

KAIMU ABDI MKENYEGE
*Mkurugenzi Mkuu*